

Maswali

1. Nani alibishana na Musa na Haruni?
2. Mbona Kora, Dathani na Abiramu walibishana na Musa?
3. Musa alisema ni nini itafanyika?
4. Watu walikutania wapi?
5. Mungu alitaka kufanya nini?
6. Nini kilitendeka kwa Kora?
7. Nani walichomwa kwa moto?
8. Makuhani walifanyaje vyetezo vya watu waovu?
9. Mbona watu walilalamika siku ifwatayo?
10. Mbona tauni ilikoma?

Majibu

1. Kora, Dathani, Abiramu na wafuasi wao 250 walibishana na Musa.
2. Kora, Dathani na Abiramu walikuwa na wivu kwa kuona kwamba Musa na Haruni ndio wa maana katika Israeli.
3. Musa aliwaambia kwamba Mungu angeonyesha kila mtu ni nani aliyemchagua.
4. Watu walikutana kwa maskani.
5. Mungu alitaka kuwaharibu wote.
6. Kora alimezwa na ardhi.
7. Wana wa kifalme waliofuata Kora 250 waliteketezwa kwa moto.
8. Makuhani walivipondaponda vil;e vyetezo vya uvumba na kuvitumia kwa kufunika madhabahu ya Mungu.
9. Watu walilalamika kwa sababu hawakutaka Kora na watu wake wauwawe..
10. Tauni ilizuiliwa wakati Haruni alifukiza uvumba katikati ya watu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



4 Kora, Dathani na Abiramu

Marejeo

Hesabu 16

Kiini cha somo

Kuona vile Mungu alitaka Waisraeli wamsujudie na mtu yeyote asijaribu kubadilisha aliyokuwa amesema.

Maneno maalum


1. Kora, Dathani, Abiramu + wivu (kijicho) kwa Musa na Haruni
2. Vyetezo vya uvumba + kuhani walioteuliwa + Misri
3. Maskani + utukufu wa BWANA
4. Haribu + ondoka
5. Ishara za Musa + ardhi ikawameza.
6. Moto + chuma ilyofuliwa + madhabahu

4.1 Kora, Dathani Abiramu walimwonea Musa na Haruni kijicho. Wana wa kifalme 250 waliungana nao. Wakasema, “Mnadhani mtatushinda sisi? Hata nasi tunaweza kuwa kuhani. Sisi wote ni watakatifu, sio nyinyi tu.”

Musa aliona vibaya na akasema, “Kesho Mungu ataonyesha nani ndiye mtakatifu. Ataonyesha nani aliyemchagua kama kuhani ili amkaribie.”

4.2 Musa alimwambia Kora na wafuasi wake wachukue vyetezo vya uvumba wanavyo vitumia wakati wanasujudia Mungu. Aliambia Kora, “Wewe unamtumkia Mungu kwa kulinda maskani lakini kukuwa kuhani Mungu ndiye anachagua.”

Musa alijaribu kuwazungumzia Dathani na Abiramu pia, lakini walikasirika. Walitamani hawangetoka Misri eti waishi jangwani. Hawakutaka Musa awe kiongozi wao. Hii ilimkasirisha Musa. Akamwambia Mungu, “Usiwasikilize au ukubali dhabihu yao kwa sababu hawatanisikiliza.”



4.3 Siku iliyofuata Kora na wafuasi wao walijaza uvumba kwa vyetezo vyao. Waisraeli wote walienda nao maskani kukutana na Musa na Haruni, utukufu wa Mungu ulionekania kila mtu.

4.4 Mungu alisema na Musa na Haruni, “Ondokeni karibu na hawa watu ili niwaharibu wote.” Wakamwomba Mungu asiwae watu wote kwa ajili ya makosa ya mtu mmoja. Mungu akasema, “Waambie watu waondoke karibu na mahema ya watu waovu!” Kila mtu akaondoka isipokuwa Kora, Dathani, Abiramu na familia zao.

4.5 Musa alisema, “Sasa mtajua kwamba Mungu ndiye alinipa mamlaka. Ardhi ikifunguka na imeze hawa watu mtajua wamemkasirisha Mungu.” Papo hapo ikapasuka! Ikawameza Kora na wafuasi wake. Ardhi ikafunga tena. Hakuna kilichosalia.

4.6 Tena Mungu akawasha moto ukateketeza wafuasi wengine 250. Makuhani wakachukua vyetezo vya watu hao waovu na kuvipigapiga mpaka wakalainisha hizo chuma. Wakazifunikia madhabahu ya Mungu. Hii iliwakumbusha watu wote kwamba Mungu ndiye anachagua makuhani wa kupeana maombi kwa Israeli.

4.7 Kesho yake watu walilalamika kwamba Musa na Haruni walikuwa wamewauwa watu wa utawa. BWANA aliwalitea tauni. Haruni alichukuwa chetezo cha uvumba. Akakimbia kwa wale watu waliokuwa wakifa na kuwafukizia uvumba. Tauni ilikoma baada ya watu 14,700 kukufa. Walikufa kwa sababu walijifanyia walivyopenda bila kufuata maagizo ya Mungu.